

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA MKUU WA WILAYA YA SIHA



**TANGAZO KWA WANANCHI
KUSHIRIKI ZOEZI LA SENSA YA WATU NA MAKAZI
TAREHE 23/08/2022**

MKUU WA WILAYA YA SIHA MHE. THOMAS APSON ANAWATANGAZIA WANANCHI NA WAKAZI WOTE WA WILAYA YA SIHA KUSHIRIKI KIKAMILIFU KATIKA ZOEZI LA SENSA YA WATU NA MAKAZI LITAKALOFANYIKA TAREHE 23 AGOSTI, 2022.

AIDHA, AMEWAOMBA VIONGOZI MBALIMBALI KATIKA JAMII KUHAMASISHA WANANCHI KUSHIRIKI KIKAMILIFU KUFANIKISHA ZOEZI HILI LA KITAIFA KWA MAENDELEO YA WANANCHI WA WILAYA YA SIHA NA TAIFA KWA UJUMLA.

KATIKA ZOEZI LA SENSA YA WATU NA MAKAZI MAKARANI WATAPITA KATIKA KAYA NA MAENEO MBALIMBALI YALIYOANDALIWA NA KUULIZA MASWALI YATAKAYOSAIDIA KUPATA TAKWIMU ZA KUPANGA MAENDELEO YA NCHI.

NAOMBA WANANCHI WOTE NA WAKAZI WA WILAYA YA SIHA KUTOA USHIRIKIANO KUFANIKISHA ZOEZI HILI MUHIMU.

NB. PAMOJA NA TANGAZO HILI ORODHA YA TAARIFA MUHIMU ZITAKAZOHITAJI ZOEZI LA SENSA IMEAMBATISHWA

LIMETOLEWA TAREHE 17/08/2022 NA


THOMAS C. APSON
MKUU WA WILAYA YA SIHA



MKUU WA WILAYA
SIHA.

Kiambatanisho A.

Taarifa muhimu zitakazoulizwa zoezi la Sensa tarehe 23/08/2022 zitahusu:

- ❖ Taarifa za kidemografia (umri, jinsi, hali ya ndoa)
- ❖ Taarifa za ulemavu (aina ya ulemavu, chanzo cha ulemavu)
- ❖ Taarifa za uhamaji
- ❖ Taarifa za vitambulisho vya utaifa na uhai wa wazazi
- ❖ Taarifa za elimu
- ❖ Taarifa za shughuli za kiuchumi
- ❖ Taarifa za umiliki wa ardhi na TEHAMA
- ❖ Taarifa za hali ya uzazi
- ❖ Taarifa ya vifo na vifo vitokanavyo na uzazi
- ❖ Taarifa za nyumba, hali ya umiliki wa nyumba, vifaa/rasilimali na udhibiti wa mazingira
- ❖ Taarifa za kilimo, mifugo, uvuvi na misitu
- ❖ Taarifa za majengo/nyumba
- ❖ Taarifa kuhusu anwani za makazi
- ❖ Taarifa za huduma za jamii katika ngazi ya Kitongoji/Shehia na Mtaa